EAST AFRICAN COMMUNITY






# EAC SIMPLIFIED GUIDE

## Utaratibu Uliorasimishwa kwa wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati - kuhusu biashara ya mazao ya kilimo yanayoharibika





Mwongozo huu rahisi kwa wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati uliandaliwa na Dorothy M. Tuma kutokana na maswali ya usajili pamoja na taarifa mbalimbali zilizochapishwa ambazo ziko kwenye matumizi ya umma.

# DIBAJI

Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) imeendelea kukuza ushirikiano kupitia Protokali za Ushuru wa Forodha na Soko la Pamoja. Shauku ya kuanzisha kwa ushirikiano huu wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kwa ajili ya kujenga ushirikiano wa kudumu, wenye ushindani na Kanda iliyoshikamana kwa kuuza bidhaa, kutoa huduma, kuwekeza mtaji na watu kuvuka kwa uhuru mipakani. Hivyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mkakati wake wa Maendeleo wa 6 umekusudia kuweka vipaumbele katika kushughulikia biashara na uwezeshaji wa kiuwekezaji ili kuondoa vikwazo vya kibiashara, na kuruhusi ushindani na kuondoa vikwazo vya kikodi, kuimarisha ushirikiano wa biashara ndogondogo miongoni mwa nchi wanachama na mchango wa wafanyabiashara wachanga, wadogo, na wa kati pamoja na mambo mengine.

Miongoni mwa mambo yanayokwamisha ufanisi wa kibiashara (NTB ) katika eneo hili ni pamoja na kukosekana kwa taarifa sahihi na zinazoeleweka na kufikika kuhusiana na biashara kati ya nchi na nchi. Kutokana na usuli huo, JAM kwa kushirikiana na GFA/GIZ wametunga kitabu hiki chenye taarifa zote muhimu na kutoa andiko hili rahisi ili liwe mwongozo wenye taarifa muhimu na za kisasa pamoja na sera muhimu, taratibu, matakwa aumahitaji, sheria za uasilia kodi, ushuru, msamaha wa kodi, vifaa vinavyohitajika ili mtu avuke mpaka kwa ajili ya wafanyabiashara wachanga, wadogo, na wa kati (MSME) ili waweze kufanya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jumuiya ya Afrika Mashariki inachukua fursa hii kuwashukuru wadau wao Federal Republic of Germany, kupitia Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) chini ya usimamizi wa GIZ-EAC Support to East African Market-Driven and People Centered Integration Programme (SEAMPEC) kwa kuwezeshwa na Regional Industrial Value Addition Project (RIVA) kwa ajili ya msaada wa kiufundi na kifedha uliotolewa kwa ajili ya kujiandaa kitabu hiki kilichorahisishwa kwa ajili ya wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati kuhusiana na kibiashara za mazao ya kilimo yanayoharibika, mifugo na mazao yanayotokana na hayo.

Tunafuraha kubwa sana kwa wataalamu wa masuala ya jinsia, kilimo, biashara, ushuru, na viwanda kutoka katika nchi washiriki kwa kushiriki kwao katika maandalizi ya mwongozo huu.





**Mh. Dk. Peter Mathuki**
**Katibu Mkuu**
**Jumuiya ya Afrika Mashariki**

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| | Dibaji | i |
| | Utangulizi | iii |
| 1 | Jumuiya ya Afrika Mashariki | 1 |
| 2 | Uwezeshwaji Wa Kibiashara– Wa Haraka Na Rahisi | 2 |
| 3 | Nyaraka  Zinazohitajika | 12 |
| 4 | Hatua Za Kusafirisha/Kuingia Bidhaa Katika Jumuiya Ya Afrika Mashariki | 27 |
| 5 | Taarifa Muhimu Za Kodi | 35 |
| 6 | Nyaraka Za Kusafiria Zilizothibitishwa | 37 |
| 7 | Mwongozo  Wa Shirika La Afya Duniani Juu Ya Uviko-19 | 38 |
| 8 | Mahali Pa Kupata Msaada | 39 |


# Finyazo

| | |
|---|---|
| AEO | Authorized Economic Operator |
| COMESA | Common Market of Eastern and Southern Africa |
| COO | Cheti cha Uasilia *Certificate of Origin* |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) |
| MSME | Wafanyabiashara Wachanga, Wadogo, na wa Kati *Micro, Small and Medium Enterprise* |
| OSBP | Kituo Kimoja cha Mpakani *One Stop Border Post* |
| SCOO | Cheti cha Uasilia Kilichorahisishwa *Simplified Certificate of Origin* |
| STR | Taratibu za Kibiashara Zilizorahisishwa *Simplified Trade Regime* |
| WCO | Shirika la Forodha Duniani *World Customs Organization* |

# UTANGULIZI

Tangu kuanza kwake Julai 2000, Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) imeendelea kutafuta namna ya kuimarisha mazingira ya kuwezesha utangamano wa Jumuiya. JAM imetekeleza jitihada kadhaa ili kukuza ushirikiano ili kuruhusu biashara na huduma kuvuka mipaka bila ya kuwapo kwa kikwazo chochote mipakani.

Hata hivyo, pamoja na juhudi zote hizo hapo juu bado kuna kikwazo kikubwa kwa biashara ambazo ni changa, ndogo na za kati (MSME) katika kuzipata taarifa na kuzielewa zinazohusiana na fursa mbalimbali za kibiashara na huduma zinazopatikana katika nchi wanachama. Wafanyabiashara wanapata ugumu wa kuzipata taarifa za kibiashara na kuweza kuzielewa. Pia wafanyabiashara wanapata ugumu kujua ni bidhaa gani na huduma gani zipo katika nchi wanachama, vigezo husika pamoja na kufahamuna namna ya kupata cheti cha ithibati, kodi, na ushuru unaotakiwa kulipwa katika kila nchi mwanachama, pamoja na sheria za kuingiza bidhaa nchini na kuzipeleka nje ya nchi, michakato ya kibiashara na udhibiti, na ufafanuzi wa mwingine ambao ni muhimu katika kufanikiwa, kujua sheria za uasilia na taratibu za kiushuru; kwa hiyo hayo ni muhimu kutoa andiko hill kwa ajili ya kufanikisha biashara za wafanyabiashara hawa kwa kuwa hawajui waende wapi kwa ajili ya kupata msaada wa kibiashara. Zaidi ya yote, wafanyabiasha pia hawajui pa kwenda kwa ajili ya kupata msaada wanapokumbana na changamoto na pia hawajui wapeleke wapi malalamiko yao.

Kwa hiyo inatakiwa kutoa andiko hili jepesi la kuwajulisha taratibu za kibiashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kanuni na maelekezo kuhusu biashara ya mazao ya kilimo yanayoharibika kwa kuwa itawasaidia wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati (MSME) waweze kufahamu ni nani wanaofanya biashara hizi katika hizi nchi. Mwongozo huu unalenga kwenye mazao na vitu vya kilimo vinavyoweza kuharibika (matunda freshi, mboga za majani, mizizi na mbegu) mifugo ya wanyama wa kufungwana aina mbalimbali za ndege/kuku na mazao yanayotokana nayo (nyama, vyakula vya nyama, mayao, na maziwa).

1

# JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) ni ushirikiano wa kikanda na kiserikali wa Jamhuri ya Burundi, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini, Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo makao yake makuu yako Arusha nchini Tanzania,

Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulisainiwa tarehe 30 Novemba mwaka 1999 na ukaanza kutumika tarehe 7 Julai, mwaka 2000.

Tangu wakati huo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeanzisha Protokali zifuatazo:

1. Protokali ya Ushuru wa Forodha The Customs Union Protocol (2005) – kwa ajili ya kurahisisha bidhaa kuvuka mipakani bila kikwazo

2. Protokali ya Soko la Pamoja The Common Market Protocol (2010) – kwa ajili ya kurahisisha wafanyakazi, watu, huduma na mitaji ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

3. Protokali ya Sarafu Moja The Monetary Union Protocol (2013) – ambayo itasababisha kuwa na sarafu ya aina moja katika JAM

Nchi washirika wa JAM pia wanaazimia kuanzisha Shirikishi la Kisiasa la Nchi za Afrika Mashariki Political Federation of East African Countries kwa siku zijazo/siku za usoni.

# 2

# UWEZESHAJI WA KIBIASHARA–URAHISI NA WEPESI

Nchi za JAM zimeweka mambo mbalimbali ya kuhakikisha ufanyaji wa biashara unakuwa ni rahisi na kuna wepesi ndani ya nchi wanachama wa JAM. Ili kufaidi mbinu zote hizo zilizowekwa, inatakiwa mfanyabiashara awe na kampuni iliyosajiliwa. Baadhi ya mbinu za uwezeshaji wa kibiashara zimeorodheshwa hapa chini:

## 1. Kituo Kimoja Cha Mpakani / *One Stop Border Posts*

Kituo Kimoja Cha Mpakani *One Stop Border Posts (OSBP)* ni mfano mmojawapo ya hatua za uwezeshaji wa kibiashara zilizoanzishwa ili kurahisisha biashara kati ya nchi washirika wa JAM. Kituo Kimoja cha Mpakani OSBP kinarejelea kwenye mipango mbalimbali ikiwemo (sheria, muundo au utaratibu wa uwakala pamoja na michakato) ambayo Nchi Washirika wa JAM zimekubaliana na kuweka mikakati ya kuwezeshabidhaa, watu na vyombo vya usafiri vinavuka kwenye mpaka wa pamoja kwa nchi zote washirika wa JAM, katika jengo moja (au kifaa kimoja) wanapoondoka eneo moja na kuingia eneo jingine la nchi mwanachama na kupitia kwenye mpaka wa pamoja.

Wakala wa Serikali zote wanao wajibu wa kutimiza/kutekeleza kwa ajili ya kusimamia mipaka katika vipengele vya (forodha, Uhamiaji, Afya, Viwango vya ubora na/vigezo vinavyohusika kilimo n.k.) ili kuwepo katika jengo moja, na ofisi hizi ni kutoka katika nchi zote za jirani (nchi wanachama).


Kituo Kimoja cha Mpakani OSBP kimepunguza muda unaotumika mpakani na kurahisisha michakato ya usajili. Badala ya kuwa na vituo viwili tofauti katika mpaka wa nchi mbili katika pande mbili tofauti za mpaka, wafanyabiashara wanavuka kupitia mpaka mmoja na wanahitaji kusimama mara moja tu kwenye Kituo Kimoja cha Mpakani OSBP katika nchi wanazokwenda.

Kwa mfano, unaposafiri kutoka Uganda kwenda Kenya kupitia mpaka wa Busia, utahitaji kusafiri na kupitia katika Kituo Kimoja Cha Mpakani OSBP. Hutahitaji kusimama Busia-Uganda Na badala yake, utakwenda moja kwa moja hadi kwenye mpaka wa pamoja wa Busia-Kenya OSBP, ambapo utakutana na wawakilishI na mawakala kutoka mpaka wa Kenya na Uganda kwenye jengo moja. Kila Kituo Kimoja Cha Mpakani OSBP kinakabiliana na foleni. Mpaka wa

Busia-Kenya OSBP unatimiza majukumu kwa ajili ya wote wanaoingia nchini Kenya. Kwa hiyo mpaka wa Busia-Uganda OSPB utashughulikia majukumu ya watu wote wanaoingia Uganda. Taratibu za kutoka nchini au kuingia nchini zinakamilishwa katika jengo moja, na kurahisisha uvukaji wa mipaka kwa urahisi na kwa haraka. Kuna mifano hapa chini na kuna aina tofauti za vituo.


## Vituo viwili vya asili vya mpakani

Watu na magari yanasimama katika vituo viwili tofauti vilivyopo katika nchi mbili tofauti kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kuvuka mpaka



## Kituo kilichounganishwa Cha OSBP (Kituo kimoja Cha mpakani kwenye Kila mpaka)


- Kupitia modeli hii nchi A na nchi B wanashirikiana kituo kimoja cha mpakani kwenye nchi moja.
- Maafisa kutoka nchi zote mbili wanakuwepo kwenye jengo moja.
- Wasafiri na magari yanasimama kituo kimoja cha mpakani. Taratibu za kutoka zinakamilishwa kabla ya kujaza taarifa za kuingia.
- Kwa mfano, mpaka wa Taveta Kenya / Holili Tanzania na mpaka wa Tanzania, Malaba Kenya / Malaba Uganda na mpaka wa Busia Kenya




| Nchi A | Kituo Kilichounganishwa cha OSBP (Juxtaposed OSBP) | Nchi B |
|---|---|---|
| Kenya | Taveta / Holili | Tanzania |
| Kenya | Malaba | Uganda |
| Kenya | Busia | Uganda |

## Kituo kilichokwama Cha OSBP (mpaka wa pamoja unaotumiwa na wote mpakani)


- Kupitia modeli hii nchi A na nchi B wanashirikiana kituo kimoja kilichopo kila upande wa mpaka.
- Wasafiri na magari yanasimama kituo kimoja cha mpakani. Taratibu za kutoka zinakamilishwa kabla ya kujaza taarifa za kuingia..
- Kwa mfano, Nemba Burundi na Gasenyi Rwanda.




| Nchi A | Kituo kilichokwama Cha OSBP (Straddled OSBP) | Nchi B |
|---|---|---|
| Burundi | Nemba/ Gasenyi | Rwanda |

## Kituo kimoja Cha mpakani OSBP (Kituo cha pamoja cha mpakani ndani ya nchi moja)

- Kupitia modeli hii nchi A na nchi B wanashirikiana kituo kimoja cha mpakani kwenye nchi moja tu.
- Maafisa kutoka nchi zote mbili wanakuwepo kwenye jengo moja.
- Wasafiri na magari yanasimama kituo kimoja cha mpakani. Taratibu za kutoka zinakamilishwa kabla ya kujaza taarifa za kuingia.
- Kwa mfano, Ruhwa Burundi katika mpaka na Rwanda.





| Nchi A | Kituo kimoja Cha mpakani OSBP (Wholly located OSBP) | Nchi B |
|---|---|---|
| Burundi | Ruhwa in Burundi | Rwanda |

## 2. Dirisha Moja la Kielektroniki / *The Single Electronic Window*

Dirisha hili ni maalumu tu kwa kampuni zilizosajiliwa, kupitia Dirisha Moja la Kielektroniki kitaifa linarahisisha upakiaji wa taarifa na nyaraka za kusafirisha/kuingiza bidhaa na ni muhimu kwa ajili ya kusafirisha/kuingiza bidhaa na mahitaji ya kuvuka mpaka kwa kuingia nchi nyingine kwa kupitia kwenye kituo kimoja cha mpakani, kwenye mfumo huu wa kimtandao ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za pande zote mbili zinazohusisha mchakato wa uingizaji bidhaa ndani ya nchi/usafirishaji bidhaa nje ya nchi. Hii inaondoa usumbufu wa kuzunguka kutoka ofisi moja na kwenda ofisi nyingine na hivyo kupunguza muda wa kushughulikia nyaraka na kuziidhinisha.

Mara taarifa husika zinapokuwa zimeingizwa kwenye mfumo (mara nyingi mawakala wa usajili), platifomu ya mtandaoni inashirikisha upakiaji wa taarifa na nyaraka kwenye mamlaka husika za kibiashara. Mamlaka tofauti za usajili wanaweza kukamilisha jukumu hili muhimu la kuidhinisha mchakato na kuchakatwa kimtandao. Wahusika wote kwenye biashara kwa nchi washirika (mfano wakala wa Serikali - ofisa wa Forodha, wakaguzi wa afya na usalama – pamoja na mawakala wa usajili, usafirishaji, mashirika ya ndege, mabenki, wasafirishaji wa bidhaa nje ya nchi na kuingiza bidhaa nchini) wanaweza kuzifikia taarifa za kiusalama na za nyaraka (pamoja na uidhinishaji), kupitia platifomu moja ya kimtandaoni ili kukamilisha michakato ya usajili ambayo inatakiwa kukamilishwa.

# ELECTRONIC SINGLE WINDOW



## 3. Mamlaka za Kuidhinisha Uchumi/ *Authorized Economic Operators (AEOs)*

Shirika la Forodha Duniani The World Customs Organization (WCO) ni Shirika la kimataifa, linalojisimamia, linalohusiana na Serikali mbalimbali ambalo kazi na lengo lake ni ni kuona kwamba utawala na usimamizi wa Ushuru wa Forodha unaongeza ufanisi na ubora katika utendaji wake wa kazi kwa maneno mengine, Shirika la Forodha Duniani linawasaidia wanachama masuala ya Forodha usimamizi/utawala wa Forodha na umeboresha utendaji kazi kupitia majukumu yao huku wakisimamia gharama zake. Mamlaka za Mapato za nchi washirika wa JAM wote ni wanachama wa Shirika la Forodha Duniani.

Kiunzi kinachotumiwa na Shirika la Forodha Duniani kwenye masuala ya biashara The WCO Framework of Standards to Secure and Facilitate Trade ambacho pia kinajulikana kama SAFE na pia kiunzi cha viwango Framework of Standards kinaelezwa kuwa ni mamlaka ya kiuchumi inayoratibiwa Authorized Economic Operator (AEO) kama sehemu inayohusisha uvukaji wa bidhaa kimataifa na kuwezesha kupita mpakani bila vikwazo, katika mazingira yoyote, au kwa niaba ya utawala na usimamizi wa forodha kitaifa, ambazo ziliidhinishwa na WCO au mnyororo salama wa kibiashara equivalent supply chain security standards.

Kwa hiyo AEO ni waratibu (binafsi, kampuni au wakala) wanaohusika katika kusafirisha au kuingiza bidhaa kwamba:


1. Wamesajiliwa kisheria kufanya biashara katika nchi zao
2. Ni walipa kodi
3. Wanaratibu shughuli za kusafirisha/kuingiza bidhaa kwa kuzingatia viwango vya Shirika la Forodha Duniani
4. Wameomba kwenye mamlaka ya Forodha nchini kwa ajili ya kuidhinishwa na AEO na kupata kibali au ithibati. Vigezo hivyohivyo vinatumikaka ili kubaini AEO katika nchi zote washirika za JAM.

AEO inajumuisha wazalishaji, wafanyabiashara, waingizaji bidhaa, wasafirishaji bidhaa, madalali, wabebaji mizigo, uunganishaji, watu wa katikati, bandarini, viwanja vya ndege, maopareta wa viwanja vya ndege, maopareta wa nchi wanachama, maghala.

Kwa kuongezea, kuna uharaka wa taratibu za kiusajili kwa, waliothibitishwa na AEOS kwa kuwa wanapata kipaumbele kwenye usajili wa mizigo, msamaha wa dhamana na ulipaji wa haraka wa madai ya fedha inayotakiwa kurudishwa.

## 4. Poto ya Taarifa za Biashara/ *Trade Information Portals*

Poto ya mtandaoni ya taarifa za kibiashara inakupa mwongozo wa hatua kwa hatua wa kukuelekeza kuhusu leseni, vibali vya muda kabla ya kusajiliwa, mahitaji ya usajili, huduma kwa wateja/dawati la usaidizi pamoja na ufikikwaji wa mfumo wa taifa wa kuripoti kuhusu vikwazo visivyohusiana na Forodha Non-Tariff Barriers (NTB). Poto ya Kikanda ya JAM inatoa taarifa na imeunganishwa na Poto za kila nchi mwanachama zinazohusiana na Poto za taarifa za Kila nchi mwanachama. Kwa maelezo Zaidi tembelea wavuti huu hapa chini wa The regional EAC Trade Portal Information Portal (https://tradehelpdesk.eac.int/).




Wafanyabiashara wenye miamala mikubwa ambayo haikidhi vigezo vya utaratibu uliorahisishwa kwa wafanyabiashara Simplified Trade Regime hutatafuta taarifa nyingi kwenye poto ya taarifa.

## 5. Utaratibu wa Kibiashara Uliorahisishwa/ *The Simplified Trade Regime*

Utaratibu wa kibiashara ulioorahisishwa unakusudia kuleta urahisi na uharaka wa kupata huduma kwa wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati katika mipaka pamoja na mazao yao ya yanaota au yanazalishwa katika JAM (kwa maneno mengine, nibidhaa za asili za Jumuiya ya Afrika Mashariki) na kuwezesha kufanya biashara na nchi nyingine wanachama wa JAM.

**STR inatumika kwa wafanyabiashara wenye mtaji sawa na au chini ya Dola 2,000 za Kimarekani**

# 3

# NYARAKA ZINAZOHITAJIKA

Wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa au wanaosafirisha bidhaa za mazao ya kilimo yanayoharibika ambao ni wazawa wa Afrika Mashariki na wanataka kufanya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaweza kuangukia katika makundi mawili kati ya haya: Kategoria namba 1 ambayo mtaji wao ni sawa na Dola za Marekani 2000 au chini ya hapo kwa thamani yake; na 2: mtaji wake ni zaidi ya Dola za Marekani 2000 kwa thamani.

Wafanyabiashara ambao mtaji wao ni Dola za Marekani 2,000 au chini ya hapo wanakidhi kigezo cha kufanya biashara chini ya utaratibu wa kibiashara uliorahisishwa Simplified Trade Regimes. Wafanyabiashara ambao mtaji wao ni zaidi ya Dola za Marekani 2,000 wnafuata taratibu rasmi zilizowekwa zinazohusu kusafirisha bidhaa au kuingiza bidhaa ndani ya JAM.

Wafanyabiashara wote wa mazao ya kilimo yanayoharibika pamoja na mazao ya mifugo (wanyama, ndege, na mazao yao) wanatakiwa wapeleke mifugo yao kwenye mamlaka husika mpakani ili zichunguzwe kiafya.

Wakati wafanyabiashara wote wa mifugo wanatakiwa wapate vibali vya kusafirisha mifugo yao ili kujiridhisha afya zao na usalama, kigezo hiki Cha kupata nyaraka husika/vibali kitasamehewa kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na bidhaa za mazao ya kilimo ambao wanafanya biashara zao chini ya utaratibu wa kibiashara uliorahisishwa Simplified Trade Regimes.

Wafanyabiashara wanahimizwa kutafuta ni nini kinahitajika katika mipaka mahususi ambako wanatarajia kupitisha bidhaa zao kwa sababu zifuatazo:
1. Vibali vya msamaha wa hizo nyaraka havipatikani katika mipaka yote
2. Taratibu katika mpaka wowote zinaweza kubadilika wakati wowote.





Je, ni Wafanyabiashara ambao mtaji wao ni zaidi au chini ya Dola 2,000 za Marekani?

sawa na au chini ya Dola 2,000 za Marekani

zaidi ya Dola 2,000 za Marekani

Utaratibu wa Kibiashara Uliorahisishwa

Taratibu rasmi za kusafirisha au kuingiza bidhaa ndani ya JAM.

- Taratibu nyingi zinafanyika bila komputa
- Nyaraka zinaandaliwa na Afisa wa Forodha au Ofisi ya Dawati la Habari za Kibiashara

-Inachakatwa kwa njia ya kielektroniki.
- Inahitaji huduma za wakala wa kupokea na kusafirisha mizigo.

Ifuatayo hapa chini ni orodha ya nyaraka zinazohitajika:

**Nyaraka Zinazohitajika**

| Waraka | Utaratibu Uliorahisishwa kwa Wafanyabiashara | Taratibu Rasmi za Kuingiza/ Kusafirisha mzigo |
|---|---|---|
| Kibali cha kusafirisha mzigo nje ya nchi (kinatolewa na nchi inayosafirisha) | Inaweza kusamehewa kwa mazao ya kilimo | X |
| Ankara/Risitit (inatolewa na nchi inayosafirisha mzigo kwenda nje ya nchi) | X | X |
| Cheti cha Uasilia wa Bidhaa/ cheti cha uasilia wa bidhaa kwa wafanyabiashara wachanga, wadogo na wa kati (inatolewa na nchi inayosafirisha mzigo kwenda nje ya nchi) | X | X |
| Cheti cha kukidhi ubora wa bidhaa (kinatolewa na nchi inayosafirisha kwenda nje ya nchi) | Inaweza kusamehewa | X |
| Cheti cha Afya au Cheti cha Afya ya mimea (kinatolewa na nchi inayosafirisha kwenda nje ya nchi) | Inaweza kusamehewa kwa bidhaa zinazohusiana na mazao yanayoharibika ya kilimo/mazao ya kilimo | X |
| Kibali cha kuingiza mzigo toka nje au Kuingiza mtambo – kinatolewa mara tu baada kufanyika ukaguzi na kuthibitika kimekidhi ubora wa kiafya na kiusalama (kinatolewa nan chi inayoingiza mzigo | Inaweza kusamehewa kwa bidhaa zinazohusiana na mazao yanayoharibika ya kilimo/mazo ya kilimo | X |
| Cheti cha Mionzi (kinatolewa kwa migizo inayoingizwa Tanzania) | | X |
| Fomu ya Kutathmini Mizigo (Uhamiaji wan chi inayoingiza mzigo) | X | N/A |
| Kadhia ya Forodha (wakala wa usajili) | N/A | X |

**1. Kibali Cha kusafirisha Bidhaa**

Wafanyabiashara waliosajiliwa na kampuni zilizosajiliwa zinazotaka kusafirisha bidhaa zinatakiwa kujisajili na mamlaka husika nchini mwao ambazo zinahusika na wakala wa usafirishaji na kuomba kibali cha kusafirisha bidhaa zao kwenda nje ya nchi. Wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa au hawafanyi biashara zao kama wafanyabiashara rasmi hawahitaji kutimiza vigezo vilivyotajwa.

**2. Ankara ya mauzo/ Risiti**

Wafanyabiashara wanaotaka kusafirisha/ kuingiza bidhaa ni lazima wapeleke ushahidi wa thamani zao au gharama za mazao ya kilimo yanayoharibika ambayo wanataka kufanyia biashara. Hii inaruhusu: (1) Usahihi wa Kategoria ya kufanya muamala kama ni kupitia STR au kupitiataratibu rasmi za kuingiza mzigo nchini/kusafirisha nje ya nchi (2) makisio ya kodi yoyote ambayo yanatakiwa yawe yamefanywa, ikiwemo kodi ya zuio the withholding tax ambayo itatozwa wakati mizigo inaingia kwenye nchi husika.

**3. Cheti cha Uasilia wa taratibu za Kibiashara zilizorasmishwa/** *Simplified Certificate of Origin*

Cheti cha Uasilia A Certificate of Origin (COO) kinathibitisha kwamba bidhaa zilizoorodheshwa hapo ama zimetengenezwa au zimekuzwa nchini ambako wanatoa cheti cha uasilia. Kama ikithibitika mazao yaliyosafirishwa yalipandwa Kenya, Kenya itatoa cheti hicho Cha Uasilia COO ili kuthibitisha kwamba mbogamboga zilipandwa Kenya.

Cheti cha Uasilia kilichorahisishwa The Simplified Certificate of Origin (SCOO) ni fupi na rahisi kukamilisha tofauti na na toleo refu la COO. Kwa hiyo, SCOO inatumika kwa ajili ya shehena kama iko sawa na au chini ya Dola za kimarekani 2,000 kwa thamani yake. Fomu ambazo hazijajazwa za SCOO zinapatikana **bure** kwa wafanyabiashara.

Bidhaa ni lazima ziambatane na Cheti cha Uasilia Kilichorahisishwa SCOO ili ikidhi vigezo vya kisamehewa **kodi** zinapoingizwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama mfanyabiashara akidai kwamba nyanya zake alizoziingiza Rwanda zilipandwa Tanzania na hajaambatisha SCOO iliyotolewa Tanzania, kwamba mfanyabiashara atatakiwa kulipa kodi kwa bidhaa anazoziingiza nchini Rwanda.

**Kanuni za Uasilia/** *Rules of Origin*
In order to qualify for zero import duties within the EAC goods must meet at least one of the two requirements concerning their origin.

**Kanuni ya 1:** Bidhaa ni lazima ziwe zimezalishwa kwa asilimia 100ndani ya JAM, bila kutoka nje ya nchi hizo wanachama. Mifano ni pamoja na bidhaa/mazao mapya, bidhaa za madini, wanyama hai na bidhaa zinaz-otokana nao pamoja na bidhaa za mawindo au uvuvi.

**Kanuni ya 2:** Bidhaa za viwandani ambazo ni pamoja na vifaa kutoka nje lazima vipitie usindikaji wa kutosha au kubadilishwa muonekano ndani ya JAM, kama ilivyoamuliwa kwa desturi kulingana na kanuni za uasilia.

**Kanuni za Uasilia –Baadhi ya mifano**
Iwapo msindikaji ataagiza juisi ya machungwa nje ya JAM na akaipeleka hadi Kenya, akaongeza sukari, akapakia tena juisi ya machungwa na kusafirisha juisi hiyo ya machungwa mpaka Rwanda, juisi hiyo iliyotiwa/iliyowekwa sukari haitakuwa na vigezo kuwa imetoka ndani ya JAM. Uongezaji wa sukari na upakiaji mpya nchini Kenya haitoshi kwa juisi hiyo ya machungwa kuchukuliwa kama ni ya kiasili na kwamba imetengenezwa ndani ya JAM. Juisi ya machungwa itavutia shughuli na kazi ya usafirishwaji itakapoingizwa nchini Rwanda.

Kwa upande mwingine, ikiwa kampuni ya kusindika juisi ya machungwa nchini Kenya itatengeneza juisi ya machungwa kwa kutumia machungwa yaliyolimwa Kenya na kuagiza rangi ya chakula ya chungwa ili iongezwe kwenye juisi ya machungwa kutoka nje ya JAM, watapakia/ na watafunga juisi ya machungwa na kuisafirisha nchini Rwanda, kutokana na asili ya machungwa na kiwango cha usindikaji kilichotokea nchini Kenya, juisi ya machungwa itachukuliwa kuwa ya asili ya Kenya na itapata msamaha wa kodi itakaposafirishwa kwenda nchini Rwanda.

**Ni Wapi pa kupata Cheti Kilichorahisishwa cha Uasilia SCOO kwenye mipaka**

Fomu zinaweza kupatikana kutoka kwenye ofisi za forodha, vyumba vya biashara, dawati la habari za kibiashara na taarifa za mipakani, na katika baadhi ya vituo ambapo forodha imeidhinisha utaratibu huo, kutoka kwenye vyama vya wafanyabiashara wanaovuka mipaka (k.m. kule Busia, Uganda).

| Nchi | Wakala Mipakani/Wakala kwenye mipaka | Gharama ya Fomu ya SCOO |
|---|---|---|
| Burundi | Mamlaka ya mapato Burundi | Hakuna |
| Kenya | Mamlaka ya mapato Kenya | Hakuna |
| Rwanda | Mamlaka ya mapato Rwanda | Hakuna |
| Tanzania | Mamlaka ya mapato Tanzania kupitia mawakala wa usambazaji | Hakuna |
| Uganda | Mamlaka ya mapato na COMESA Dawati la Taarifa za Biashara | Hakuna |
| Sudani Kusini | Haijatekelezwa wakati wa kuchapisha miongozo hii | N/A |

Ingawa hakuna malipo ya kupata fomu za SCOO, Dawati la Taarifa za Biashara linaweza kutoza kwa mchakato wa kujaza fomu ya SCOO kwa niaba ya mfanyabiashara. SCOO inatolewa kwa kila muamala na haiwezi kutumika zaidi ya mara moja.

SCOO zilizokamilika huthibitishwa na kuidhinishwa na ofisi ya forodha nchini, mazao ya kilimo yaliyopandwa humo, pia itajulikana kama nchi ya kusafirisha nje ya nchi.

# Sampuli ya SCOO ya JAM

**EAST AFRICAN COMMUNITY SIMPLIFIED CERTIFICATE OF ORIGIN**

(For goods of a value not exceeding US $ 2000)

*(Kwa bidhaa zenye thamani isiyozidi US$ 2000)*

<table>
<tr><td>1) Exporter (name, full address, country)<br><br>Msafirishaji (Jina na Anwani)</td><td colspan="2">Reference Number ……………<br><br>Kumb Na</td></tr>
<tr><td>2) Importer (Names & address)<br>Mwingizaji Bidhaa,( Jina na anuan yakei)</td><td colspan="2">3)Country of Origin<br>Uthibitisho wa Uasili wa Bidhaa</td></tr>
<tr><td>4)Description of goods<br>(Maelezo ya Bidhaa)</td><td>5)No. and type of packages<br>Namba na aina ya kifurushi</td><td>6)Value<br>Thamani</td></tr>
<tr><td>7)Declaration by Exporter/Importer<br>Tamko la Msafirishaji/Mzalishaji/Mgavi<br><br>I, the undersigned Mr/Mrs/Ms………………………….. declare that the goods described above have been produced in (country) ………………………..in accordance with the EAC Rules of Origin.<br><br>Signature………………………………………<br>(Saini)<br>Place……………………………………………<br>(Mahali)<br>Date…………………………………………<br>(Tarehe)<br>Official stamp<br>(Mhuri)</td><td colspan="2">8)Customs Endorsement<br>(Uthibitisho wa Forodha)<br><br>I, the undersigned, hereby endorse the exporters' declaration and certify that the goods qualify under the EAC Rules of Origin.<br><br>Signature………………………………………<br>(Saini)<br>Place……………………………………………<br>(Mahali)<br>Date……………………………………………<br>(Tarehe<br>Official stamp<br>(Mhuri)</td></tr>
</table>

## 4. Nyaraka za Afya na Usalama

Kuna idadi ya nyaraka za afya na usalama zinazotakiwa.

### 4.1 Cheti cha Makubaliano

Cheti cha Makubaliano hutolewa na Ofisi ya Kitaifa ya Viwango vya Ubora katika nchi inayosafirisha bidhaa kwenda nje ya nchi. Inathibitisha kuwa bidhaa zinazosafirishwa zimejaribiwa, zinakidhi viwango vya ubora vilivyoidhinishwa vya kitaifa na ni salama kwa matumizi ya binadamu, nyama iliyosindikwa na kufungwa, bidhaa za nyama na maziwa lazima zifikie viwango vya ubora vinavyohitajika. Hili ni hitaji ambalo haliwezi kuachwa.

Ofisi ya Taifa ya Viwango vya Ubora katika baadhi ya vituo vya mipakani ndani ya JAM zina vifaa vya maabara kwaajili ya kufanya vipimo muhimu. Katika baadhi ya vituo vya mipaka, sampuli za vifaa hutumwa kwenye maabara ya Ofisi ya Taifa ya Viwango vya Ubora katika mji mkuu, jambo ambalo husababisha ucheleweshaji.

| Nchi | Wakala | Ada |
|---|---|---|
| Burundi | Ofisi ya Viwango na Udhibiti wa Ubora wa Burindi | Ada ya vipimo inatofautiana kulingana na bidhaa (wasiliana na wakala husika |
| Kenya | Ofisi ya Viwango (KEBS) | |
| Rwanda | Bodi ya viwango (RSB) | |
| Tanzania | Ofisi ya viwango Tanzania (TBS) | |
| Uganda | Ofisi ya Taifa ya viwango Uganda (UNBS) | |
| Sudani Kusini | Ofisi ya Taifa ya Viwango Sudani ya Kusini (SSNBS) | |

## 4.2 Cheti cha Usafi wa mimea / *Phytosanitary Certificate*

Cheti cha usafi wa mimea Phytosanitary inathibitisha kwamba bidhaa za (mimea, mbegu na matunda) zilizoelezwa kwenye cheti hazina wadudu na magonjwa ya mimea.

Mkaguzi aliyeidhinishwa amegundua kuwa mazao ni:

(a) yamefungashwa ipasavyo katika vifungashio visivyo na wadudu

(b) bila wadudu, magonjwa au magugu

Wafanyabiashara wanaofanya kazi chini ya STR hawahitaji kupata cheti cha usafi wa mimea. Walakini, bidhaa wanazouza nje zinapaswa kukaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa.

Cheti cha usafi wa mimea kinaweza kupatikana kutoka kwenye mashirika yaliyoidhinishwa, ambayo yameorodheshwa hapa chini kama ifuatavyo katika nchi tofauti za JAM. Tozo zinazotozwa katika kila nchi kufikia Septemba 2021 zimetolewa pia.

| Nchi | Wakala | Ada |
|---|---|---|
| Burundi | Idara ya Ulinzi wa Mimea (Wizara ya Mazingira, Kilimo na Mifugo) | |
| Kenya | Huduma ya Ukaguzi wa Afya ya Mimea Kenya (KEPHIS) | KES 1,000 (inatofautiana) |
| Rwanda | Kitengo cha Ukaguzi na Udhibiti (MINAGRI) | RWF 2,000 |
| Tanzania | Kitengo cha Taifa cha Usalama wa Chakula (Wizara ya Kilimo) | TZS 35,700 |
| Uganda | Huduma za Ukaguzi wa Mimea (Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi) | UGX 5,000 (maombi)<br>UGX 20,000 (ukaguzi) |
| Sudani Kusini | South Sudan National Bureau of Standards | |

## 4.3 Cheti cha Afya ya Mnyama

Cheti cha Afya ya Mnyama *national veterinary services* kinatolewa na mamlaka iliyoidhinishwa ya kitaifa inayohusika na huduma za wanyama kupitia ama Kurugenzi ya Huduma za Wanyama *Directory of Veterinary Services* au Wizara inayoshighulikia mambo ya mifugo *(angalia jedwali hapa chini li uone orodha ya mamlaka husika za afya pamoja na za usalama wa mifugo katika JAM)*. Hakuna msamaha wa ukaguzi kwa mifugo au ndege wanaoingizwa ni lazima kupata kibali.

## 4.4 Cheti cha Kuingiza Mifugo/Ndege au Kibali / *Import Certificate or Permit*

Cheti cha Kuingiza (kibali) kinatolewa na mamlaka ya kiserikali iliyoidhinishwa na nchi inayoingiza inathibitisha kwamba bidhaa zinazotajwa kwenye cheti (kibali) zinakidhi vigezo vya kiafya  na usalama na mahitaji ya kimazingira na afya ya mimea na ni salama kwa matumizi ya binadamu.

